

## HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO

### MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 05/11/2021 KWENYE OFISI YA MKURUGENZI MVUHA

#### Wajumbe Waliohudhuria:

- |                               |                                 |
|-------------------------------|---------------------------------|
| 1. Mh. Lucas Jaji Lemomo      | - Mw/kiti. Halmashauri          |
| 2. Ndugu Rehema S. Bwasi      | - Mkurugenzi - Katibu           |
| 3. Mh. Hamisi Issa Msangule   | - Makamu Mw/kiti wa Halmashauri |
| 4. Mh. Maulid M. Mkangu       | - Mjumbe                        |
| 5. Mh. Yahya H. Mfaume        | - Mjumbe                        |
| 6. Mh. Jesca J. Mbondo        | - Mjumbe                        |
| 7. Mh. Mwajuma R. Hobwe       | - Mjumbe                        |
| 8. Mh. Ally A. Mwamilang'anga | - Mjumbe                        |
| 9. Mh. Mwinyi Y. Bui          | - Mjumbe                        |
| 10. Mh. Charles P. Mboma      | - Mjumbe                        |
| 11. Mh. Pendo Hassani Mghwai  | - Mjumbe                        |
| 12. Mh. Amiri A. Mihungo      | - Mjumbe                        |

#### Wajumbe wasiohudhuria

- |                                |          |               |
|--------------------------------|----------|---------------|
| 1. Mh. Hamisi S. Taletale (Mb) | - Mjumbe | - Kwa taarifa |
| 2. Mh. Innocent Kalogeris (Mb) | - Mjumbe | - kwa taarifa |

#### Wataalam Waliohudhuria.

- |                             |   |
|-----------------------------|---|
| 1. Ndugu Ogunde S. W.       | - Kaimu Afisa Utumishi (W)                        |
| 2. Ndugu Ndelisho H. Moshi  | - Afisa Mifugo na Uvuvi (W)                       |
| 3. Ndugu Agatha Semgoja     | - Kaimu Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W) |
| 4. Ndugu Charles Komba      | - Mhasibu wa mapato                               |
| 5. Ndugu Salehe Mbogoso     | - Mhasibu wa mapato                               |
| 6. Ndugu Patrick Mwakilili  | - Afisa Ardhi (W)                                 |
| 7. Ndugu Rosemary Semiono   | - Kaimu Afisa Mazingira (W)                       |
| 8. Ndugu Frolence Mwambene  | - Afisa Maendeleo ya Jamii (W)                    |
| 9. Ndugu Lusajo Hosea       | - Kaimu Mkaguzi wa Ndani (W)                      |
| 10. Ndugu Ester Edward      | - Kaimu mwanasheria (W)                           |
| 11. Ndugu Nicholas Mwaihojo | - Kaimu Afisa Maliasili (W)                       |
| 12. Ndugu Joshua Chilonwa   | - Kaimu Afisa Elimu Msingi (W)                    |
| 13. Ndugu Grace L. Nyabange | - Afisa Manunuzi (W)                              |
| 14. Ndugu Ephraim Shapanga  | - Afisa TEHAMA (W)                                |
| 15. Ndugu Juma A. Chimwaga  | - Mhandisi wa Ujenzi (W)                          |
| 16. Ndugu Kasole E. Maungo  | - Kaimu Mganga Mkuu (W)                           |
| 17. Ndugu Eustaki Moshi     | - Mratibu wa TASAF                                |
| 18. Ndugu Eliaza E. Kidjout | - Mweka Hazina                                    |



- |                               |                          |
|-------------------------------|--------------------------|
| 19. Ndugu Tajiri Kihemba      | - Kaimu Afisa Habari (W) |
| 20. Ndugu Eliwangu Mzava      | - Kaimu Afisa Nyuki (W)  |
| 21. Ndugu Amandus U. Chimwaga | - Afisa Usafirishaji (W) |
| 22. Ndugu Salifu E. Venance   | - Afisa Mipango (W)      |

**Sekretarieti**

- |                             |                      |
|-----------------------------|----------------------|
| 1. Ndugu Mganga A. Semwija  | - Mwandishi wa Vikao |
| 2. Ndugu Michael J. Malindi | - Mwandishi wa Vikao |

**Muht. Na. 03/01/11/2021 - Kufungua kikao**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao. Mwenyekiti aliwaalika wajumbe kwenye kikao cha kamati ya Fedha, Utawala na Mipango kupitia taarifa za mwezi Septemba kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 kisha baada ya kusema hayo alifungua kikao mnamo saa 04:21 asubuhi.

**Muht. Na. 03/02/11/2021 - Kuridhia Ajenda:**

1. Kufungua Kikao
2. Kuridhia ajenda
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango wa tarehe 20/09/2021
4. Kupitia yatokanayo na kikao cha kamati ya Fedha, Utawala na Mipango cha tarehe 20/09/2021.
5. Kupitia taarifa ya mapato na matumizi kwa mwezi Septemba 2021/2022.
6. Mapendekezo ya kufanya marekebisho ya baadhi ya vyanzo vya mapato.
7. Kupitia taarifa ya Mkaguzi wa Ndani ya Robo ya kwanza kwa mwaka wa Fedha 2021/2022.
8. Kupitia taarifa za utekelezaji wa idara na vitengo kwa robo ya kwanza
  - i. Idara ya Utumishi na Utawala.
  - ii. Kitengo cha Sheria.
  - iii. Kitengo cha Manunuzi.
  - iv. Kitengo cha Tehama.
9. Taarifa ya Utekelezaji ya Miradi ya Maendeleo kwa Kipindi cha robo ya kwanza.
10. Taarifa ya fedha za Mpango wa maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO - 19 Halmashauri ya Wilaya Morogoro.
11. Ujenzi wa vituo vya Afya viwili vipya.
12. Taarifa ya maandalizi ya Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022.
13. Taarifa ya kikao cha kamati ya mikopo kilichofanyika tarehe 12/10/2021.
14. Taarifa ya uhakiki wa maeneo yaliyotolewa kwa kampuni ya Morogoro Sugar kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo cha miwa.
15. Maombi ya mkopo wa fedha Tshs 865,210,000 za miradi ya upimaji viwanja katika miji ya Ngerengere na Kisaki
16. Mfumo mpya wa urasimishaji makazi kupitia mikopo ya NMB.



17. Taarifa ya ziara ya Kamati ya Fedha kukagua miradi ya maendeleo robo ya kwanza kwa mwaka 2021/2022
18. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti
19. Kufunga kikao

### **Hitimisho**

Wajumbe baada ya kusoma kwa makini waliridhia ajenda zilizowasilishwa ndizo zilizojadiliwa kwenye kikao cha kamati ya Fedha, Utawala na Mipango cha tarehe 05/11/2021.

### **Muht. Na. 03/03/11/2021 - Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha kamati ya Fedha, Utawala na Mipango cha tarehe 20/09/2021.**

Baada ya wajumbe kupitia ukurasa kwa ukurasa muhtasari wa kikao cha tarehe 20/09/2021 waliridhia pamoja na marekebisho yake. Mwenyekiti na Katibu waliweka saina kuwa kumbukumbu halali ya Halmashauri.

### **Muht. Na. 03/04/11/2021 - Kupitia yatoakanayo na kikao cha kamati ya Fedha, Utawala na Mipango cha tarehe 20/09/2021**

Baada ya wajumbe wa kamati kupitia yatoakanayo na kikao cha kamati ya Fedha, Utawala na Mipango cha tarehe 20/09/2021. Wajumbe baada ya majadiliano waliazimia kwamba

### **Azimio**

1. Iwasilishwe orodha ya vibanda vyote, lengo kwa mwaka, amelipa kiasi gani na hatua zilizochukuliwa kwa wale wote wasiolipa kwa mwaka 2020/2021 na 2021/2022.
2. Kwa kuwa hadi sasa Jenifa Lwila amelipa Tshs 750,000/= na kuahidi kumalizia deni lake mwezi Disemba 2021 taarifa ya kumalizia deni hilo iwasilishwe katika kikao cha mwezi Disemba 2021.
3. Mtendaji Festo Kilianl Mulila aliyehamia kijiji cha Lugeni anadaiwa fedha Tshs 257,000.00 na fedha za mfuko wa jimbo taarifa zilifika katika ofisi ya Utumishi. Taarifa yake iwasilishwe katika kikao kijacho.
4. Katika kikao kijacho iwasilishwe mikataba iliyosainiwa ya mgambo wote wa magetini na fedha walizolipwa ikiwa ni pamoja na mlinzi wa geti la Madamu (*Raimu Idd Shabani*)
5. Kwa kuwa Mzabuni Bruno hajalipwa hadi awasilishe viambata kikao kiliazimia kwamba Mkurugenzi afanye mawasiliano na Bruno ili awasilishe viambata na alipwe fedha zake.
6. Ifanyike tathimini ya umalizaji wa soko la Mkuyuni hasa uwekaji wa marumaru
7. **Maazimio kutokana na Hoja za ukaguzi wa ndani robo ya nne 2020/2021**
  - i. **Hoja namba 4.1.2** Ukaguzi wa mapato kutoka vyanzo mbalimbali ambayo hayajawasilishwa benki. Kamati ilitoa wiki mbili kuanzia tarehe 20/09/2021



hadi tarehe 04/10/2021 fedha zilizosalia Tshs 2,584,980.00 kati ya deni la Tshs 5,448,130.00 ziwe zimewasilishwa benki.

- ii. **Hoja namba 4.2.1** Malipo kwa Wazabuni kiasi cha Tshs 74,307,814.00 = yaliyokosa risiti za EFD. Hadi sasa risiti zenye thamani ya Tshs 30,753,682.00 ziliwasilishwa bado risiti zenye thamani ya Tshs 43,554,140. Mweka Hazina ashirikiane na Afisa Manunuzi kuhusu ufuatiliaji wa risiti za EFD. Pia menejimenti itumie kanuni na miongozo kuhusu wazabuni wadaiwa kuwasilisha risiti za EFD.

**Muht. Na. 03/05/11/2021 - Taarifa ya Mapato na Matumizi ya mwezi Septemba kwa mwaka wa fedha 2021/2022.**

Mweka Hazina aliwasilisha taarifa ya mapato na matumizi kwa mwezi Septemba kwa wajumbe kama ifuatavyo: Aliwaeleza wajumbe kwamba kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Halmashauri ilikisia kukusanya na kupokea jumla ya Tshs. 46,640,816,137.00

**HALI HALISI**

**Mapato**

**Mhe. Mwenyekiti,**

Katika hadi kufiki mwezi Septemba 2021 Halmashauri ilipokea Jumla ya Tshs 3,778,353,150.84 sawa na asilimia 19.73 ya bajeti ya Mwaka 2021/2022. Mapato haya yamejumuisha mapato ya ndani Tshs 856,942,927.50 sawa na asilimia 45.08 ya bajeti ya mwaka 2021/2022, Mishahara toka Serikali Kuu Tshs 2,274,703,500.00 sawa na asilimia 21.10 ya bajeti ya 2021/2022, fedha za matumizi mengineyo (OC) Tshs. 49,537,499.97 sawa na asilimia 33.13 ya bajeti ya mwaka 2021/2022 na Miradi ya Maendeleo Tshs 597,169,223.37 sawa na asilimia 7.98 fedha hizi ni kwa ajili ya elimu bila malipo, ujenzi wa madarasa, kituo cha afya Kidugalo, UVIKO-19, Mabusha na Matende.

Katika kipindi cha Mwezi Septemba 2021 Halmashauri ilipokea na kukusanya jumla ya Tshs 3,778,535,150,000.00.

**Matumizi**

Kipindi cha mwezi Septemba 2021 Halmashauri ilitumia Jumla ya Tshs 2,795,817,402.00 sawa na asilimia 8.87 ya bajeti ya Mwaka 2021/2022. Matumizi haya yamejumuisha mapato ya ndani Tshs 128,093,867 sawa na asilimia 8.87 ya bajeti ya mwaka 2021/2022, Mishahara kutoka serikali kuu Tshs 2,274,578,438 sawa na asilimia 7.32 ya bajeti ya mwaka 2021/2022, Matumizi Mengineyo (OC) Tshs. 352,383,000 sawa na asilimia 17.24 ya bajeti na Miradi ya Maendeleo shs 148,050,824 sawa na asilimia 1.78 fedha hizi zimejumuisha fedha za elimu bure ambazo zimepelekwa shuleni na vifaa vya ujenzi wa hospitali ya Wilaya. Katika kipindi cha Mwezi Septemba 2021 Halmashauri imetumia jumla ya TZS 114,603,044



kuendelea kutoa habari mbalimbali kupitia tovuti ya Halmashauri ambayo ni [www.morogorodc.go.tz](http://www.morogorodc.go.tz), pamoja na mitandao mingine ya kijamii kama vile Instagram na facebook. Aidha, Kitengo kimeanza kuandaa vipindi maalumu vya Elimu kwa Umma redioni ambavyo vitaruka hewani kila juma la kwanza na la mwisho kwa kila mwezi.

### Hitimisho

Wajumbe walipokea na kuridhia taarifa za Idara na Vitengo kama zilivyowasilishwa.

### Muht. Na. 03/09/11/2021 - Taarifa ya Utekelezaji ya Miradi ya Maendeleo kwa Kipindi cha robo ya kwanza 2021/2022.

Katibu aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, aliwaeleza wajumbe kwamba katika kipindi cha robo ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Halmashauri ilitekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo iliyopokea fedha katika kipindi cha Robo ya I&II mwaka 2020/2021 na haikukamilika. Miradi iliyotekelezwa katika kipindi hiki inatokana na fedha za miradi kutoka Serikali Kuu pamoja na fedha za EP4R na TEA. Kwa upande wa fedha za Serikali kuu kiasi cha Shs.750,000,000.00 ni kwa ujenzi wa Ofisi za Utawala, Ujenzi wa wodi tatu (wanaume, wanawake na watoto) Shs.500,000,000.00, Ukamilishaji wa zahanati saba (7) Shs. 350,000,000.00 pamoja na Tsh 360,000,000.00 ukamilishaji wa maabara 12 za sekondari. Kwa upande wa EP4R Tshs 677,400,000.00 na TEA Tshs. 275,000,000.00 ni kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya madarasa, matundu ya vyoo pamoja na nyumba za watumishi.

Wajumbe baada ya kupitia taarifa ya miradi ya maendeleo waliazimia kwamba

### Azimio

Kamati ya Fedha iende kuona vyoo vilivyojengwa kwa thamani ya Tshs 40,000,000.00 shule ya Sekondari Mikese kuwa ni matundu mangapi.

### Muht. Na. 03/10/11/2021 - Taarifa ya fedha za mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVIKO- 19 Halmashauri ya Wilaya Morogoro.

Katibu aliwasilisha taarifa ya fedha za mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVIKO - 19 Halmashauri ya Wilaya Morogoro. Aliwaeleza wajumbe kwamba Katika mpango tajwa hapo juu, Halmashauri imenufaika kwa kiasi cha Tshs 3,255,709,217.00 kwa mgawanyo ufuatao

### Mchanganuo wa fedha za mpango wa UVIKO - 19

NA	ENEO LA MATUMIZI	SEKTA	IDADI	GHARAMA	JUMLA
1	Ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari	Elimu Sekondari	103	20,000,000.00	2,060,000,000.00
2	Ujenzi wa madarasa katika vituo shikizi vya shule 5 za msingi	Elimu Msingi	11	20,000,000.00	220,000,000.00
3	Ujenzi wa Jengo la huduma za dharura (EMD)	Afya	1	300,000,000.00	300,000,000.00
4	Ujenzi wa nyumba za watumishi	Afya	1	90,000,000.00	90,000,000.00



5	Ununuzi wa vifaa vya huduma ya dharula	Afya	1	571,554,000.00	571,554,000.00
6	Mafunzo	Afya	1	8,813,913.04	8,813,913.00
7	Ufuatiliaji na Tathmini	Mipango	1	5,341,304.00	5,341,304.00
	<b>Jumla</b>				<b>3,255,709,217.00</b>

Miradi yote katika Sekta ya afya iliyoainishwa (*Jengo la huduma za dharula na nyumba za watumishi*) itajengwa Hospitali ya Wilaya - Mvuhu. Fedha zilizopokelewa ni Tshs 2,280,000,000.00

#### Mapokezi ya fedha za mpango wa UVIKO -19

NA	ENEO LA MATUMIZI	SEKTA	IDADI	GHARAMA	JUMLA
1	Ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari	Elimu Sekondari	103	20,000,000.00	2,060,000,000.00
2	Ujenzi wa madarasa katika vituo shikizi vya shule 5 za msingi	Elimu Msingi	11	20,000,000.00	220,000,000.00
	<b>Jumla</b>				<b>2,280,000,000.00</b>

#### Mgawanyo wa madarasa 103 sekondari.

Mgawanyo wa madarasa umezingatia uhitaji katika shule husika hasa kwa kuzingatia wingi wa wanafunzi na mipango ya baadae katika shule husika mgawanyo huu upo kama ifuatavyo

#### Mgawanyo wa madarasa ya Sekondari.

NA	KATA	JINA LA SHULE	IDADI	KIASI	JUMLA
1	KASANGA	KIZAGILA SS	2	20,000,000	40,000,000
2	BWAKIRACHINI	BWAKIRACHINI SS	8	20,000,000	160,000,000
3	BWAKIRAJUU	BWAKIRAJUU SS	2	20,000,000	40,000,000
4	KOLERO	KOLERO SS	2	40,000,000	40,000,000
5	MVUHA	MVUHA SS	6	20,000,000	120,000,000
6	SELEMBALA	SELEMBALA SS	2	20,000,000	40,000,000
7	LUNDI	LUNDI SS	2	20,000,000	40,000,000
8	MTOMBOZI	MTOMBOZI SS	2	20,000,000	40,000,000
9	KISEMU	KISEMU SS	2	20,000,000	40,000,000
10	KONDE	MATOMBO SS	5	20,000,000	100,000,000
11	KIBOGWA	KIBOGWA SS	2	20,000,000	40,000,000
12	TAWA	TAWA SS	2	20,000,000	40,000,000
13	KIBUNGO JUU	KIBUNGO JUU SS	2	20,000,000	40,000,000
14	KISAKI	KISAKI SS	8	20,000,000	160,000,000
15	MNGAZI	MILENGWELENGWE SS	2	20,000,000	40,000,000
16	SINGISA	SINGISA SS	2	20,000,000	40,000,000
17	MKULAZI	MKULAZI SS	2	20,000,000	40,000,000
18	MATULI	MATULI SS	3	20,000,000	60,000,000
19	KIDUGALO	FATEMI SS	2	20,000,000	40,000,000
20	TUNUNGUO	TUNUNGUO SS	2	20,000,000	40,000,000
21	NGERENGERE	NGERENGERE SS	8	20,000,000	160,000,000
22	GWATA	GWATA SS	3	20,000,000	60,000,000
23	MIKESE	MIKESE SS	8	20,000,000	160,000,000
24	MKAMBARANI	NELSON MANDELA SS	8	20,000,000	160,000,000
25	TOMONDO	TOMONDO SS	3	20,000,000	60,000,000
26	KIROKA	KIROKA SS	3	20,000,000	60,000,000
27	MKUYUNI	MKUYUNI SS	6	20,000,000	120,000,000
28	KINOLE	KINOLE SS	2	20,000,000	40,000,000
29	TEGETERO	TEGETERO SS	2	20,000,000	40,000,000
	<b>JUMLA KUU</b>		<b>103</b>		<b>2,060,000,000</b>



### Mgawanyo wa madarasa kwa shule shukizi

Halmashauri ina jumla ya shule shikizi 15 lakini katika mgao huu wa madarasa 11 kipaumbele kimewekwa kwa shule shikizi 5 ambazo zimeshakaguliwa na madarasa yakijengwa taratibu za usajiri zitakamilishwa kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapa chini; -

### Mchanganuo wa vyumba vya madarasa katika vituo shikizi

NA	KATA	JINA LA SHULE	IDADI	GHARAMA
1.	Kisemu	Shule ya mkondo - Gozo iliyoko Nige	2	40,000,000.00
2.	Kwaba	Shule ya mkondo - Ngese iliyoko Kwaba	3	60,000,000.00
3.	Mikese	Shule ya Mkondo Mgama - iliyoko Muungano	2	40,000,000.00
4.		Shule ya mkondo Koo - iliyoko Mikese	2	40,000,000.00
5.	Mkambarani	Shule ya Mkondo Muunguzi - iliyoko Mkombozi	2	40,000,000.00
<b>JUMLA</b>			<b>11</b>	<b>220,000,000.00</b>

### Uingizaji wa fedha kwenye akaunti za shule.

Katika uingizaji wa fedha kuna baadhi ya shule zimefunguziwa madarasa na nyingine zimeongezewa madarasa na zipo shule ambazo hazikupata fedha kabisa, hata hivyo maelekezo yametolewa kuwa tutekeleze kulingana na fedha zilivyoingizwa kwenye akaunti na si vinginevyo. Shule zilizoingiziwa fedha ni hizi zifuatazo.

NA	KATA	JINA LA SHULE	IDADI	KIASI	JUMLA
<b>A: SHULE ZA SEKONDARI</b>					
1	Kasanga	Kizagila Ss	4	20,000,000	80,000,000
2	Bwakirachini	Bwakirachini Ss	6	20,000,000	120,000,000
3	Bwakirajuu	Bwakirajuu Ss	4	20,000,000	80,000,000
4	Kolero	Kolero Ss	2	40,000,000	40,000,000
5	Mvuha	Mvuha Ss	4	20,000,000	80,000,000
6	Selembala	Selembala Ss	2	20,000,000	40,000,000
7	Lundi	Lundi Ss	2	20,000,000	40,000,000
8	Mtombozi	Mtombozi Ss	4	20,000,000	80,000,000
9	Kisemu	Kisemu Ss	2	20,000,000	40,000,000
10	Konde	Matombo Ss	4	20,000,000	80,000,000
11	Kibogwa	Kibogwa Ss	4	20,000,000	80,000,000
12	Tawa	Tawa Ss	4	20,000,000	80,000,000
13	Kibungo juu	Kibungo Juu Ss	4	20,000,000	80,000,000
14	Kisaki	Kisaki Ss	6	20,000,000	120,000,000
15	Mngazi	Milengwelengwe Ss	2	20,000,000	40,000,000
16	Singisa	Singisa Ss	2	20,000,000	40,000,000
17	Mkulazi	Mkulazi Ss	4	20,000,000	80,000,000
18	Matuli	Matuli Ss	0	20,000,000	00
19	Kidugalo	Fatemi Ss	3	20,000,000	60,000,000
20	Tununguo	Tununguo Ss	2	20,000,000	40,000,000
21	Ngerengere	Ngerengere Ss	8	20,000,000	160,000,000
22	Gwata	Gwata Ss	3	20,000,000	60,000,000
23	Mikese	Mikese Ss	6	20,000,000	120,000,000
24	Mkambarani	Nelson Mandela Ss	7	20,000,000	140,000,000
25	Tomondo	Tomondo Ss	3	20,000,000	60,000,000
26	Kiroka	Kiroka Ss	3	20,000,000	60,000,000
27	Mkuyuni	Mkuyuni Ss	5	20,000,000	100,000,000



28	Kinole	Kinole Ss	2	20,000,000	40,000,000
29	Tegetero	Tegetero Ss	1	20,000,000	20,000,000
	<b>JUMLA KUU</b>		<b>103</b>		<b>2,060,000,000</b>
<b>B</b>	<b>SHULE SHIKIZI</b>				
1	Mvuha	Sangasanga- Mvuha	2	20,000,000	40,000,000
2		Mgama - Muungano	3	20,000,000	60,000,000
3	Mikese	Shule ya Mkondo Koo - Iliyoko Mikese	2	20,000,000	40,000,000
4	Gwata	Mavuru - Mazizi	2	20,000,000	40,000,000
5	Tununguo	Nyambogo - Kisanga Stendi	2	20,000,000	40,000,000
	<b>JUMLA</b>		<b>11</b>	<b>JUMLA</b>	<b>220,000,000.00</b>

### Hitimisho

Wajumbe walijadilana kwamba toka fedha zilipoingizwa katika Halmashauri Wah. Madiwani hawakushirikishwa. Mwenyekiti alieleza kwamba jambo hili lilikuwa ni la Kitaifa alishirikishwa Mkoani. Alieleza kwamba Kata ya Matuli awali ilikuwa na madarasa 6 kwa awamu ya pili hakuna darasa hata moja, Mkurugenzi aliandika barua kupata ufafanuzi lakini hakuna madarasa yaliyopatikana kwa kata hiyo. Mkurugenzi alieleza kwamba walipokutana na Mkuu wa Wilaya aliagiza kwamba kwenye fedha ambazo awali zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na Halmashauri Tshs 200,000,000 zitengwe kwa ajili ya Kata ya Matuli na zitakazosalia waangalie mahali pa kupeleka.

Wajumbe wa kamati ya fedha walikubaliana kwamba zitengwe fedha Tshs 60,000,000.00 ziende kata ya Matuli kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na Tshs 20,000,000.00 ziende shule ya Msingi Tegetero kwa ajili ya ujenzi wa Darasa moja ambalo fedha za UVIKO-19 hazikupelekwa.

Mh. A. A. Mwamilang'anga alieleza kwamba fedha za ujenzi wa Bweni la shule ya sekondari ya Mkuyuni na Bwakila Chini ujenzi wake ulianza pamoja lakini Mkuyuni mahitaji yalikuwa ni makubwa kwa sababu ya kuongezeka kwa ukubwa wa bweni tofauti na Bwakila Chini. Kuhusu fedha za Kiburumo Mwenyekiti aliwaeleza wajumbe kwamba fedha za Kiburumo zililiwa na mfumo ambazo zilitoka DAWASA. Hivyo madarasa yaliyojengwa yalipigwa bati na bado umaliziaji tu. Mh. M. R. Hobwe aliomba fedha zipelekwe Kiburumo kwa ajili ya kumaliza madarasa hayo. Mh. A. A. Mihungo alichangia kwamba Halmashauri ijipange kuhakikisha kwamba madarasa ya shule ya msingi Kiburumo yanajengwa kisasa. Mh. C.P. Mboma aliwaeleza wajumbe kwamba shule ya msingi Mnguzi awali walipata fedha za ujenzi wa madarasa mawili lakini kwenye mpango mpya hawakuwa na fedha zozote. Halmashauri ikipata fedha za mapato ya ndani iangaliwe shule shikizi ya Mnguzi.

Wajumbe baada ya kupitia taarifa ya mgawano wa fedha za UVIKO- 19 walikubaliana kwamba kwenye kikao cha kamati ya fedha kufanyike mgawanyo wa fedha (*allocation*).

### Fedha ya kununua gari la Halmashauri

Uwasilishwe mpango wa Halmashauri wa kununua gari jingine na Mh. A. A. Mwamilang'anga alieleza kwamba ununuzi wa gari ni muhimu kama mabadiliko yatafanyika kwenye taarifa ya ununuzi wa gari iliyoletwa mwanzo, aidha kama ununuzi wa gari jipya utaanza tena basi nivyema kuendelea na mchakato wa gari la awali ili



tusirudi nyuma. Aidha alisisitiza kuwa, Ili kuonesha thamani ya fedha tumalize baadhi ya miradi ambayo ilianzishwa na Halmashauri kama soko la Tawa, Kinole na Majimoto Kisaki. Vitega uchumi hivi vikamilishwe ili viweze kuwa ni vyanzo vya mapato.

### **Tathimini ya eneo la ujenzi wa stendi**

Mhandisi awasilishe Tathimini ya ujenzi wa stendi ya Msovinzi na Mikese na utaratibu wa utekelezaji.

### **Muht. Na. 03/11/11/2021 - Maelekezo ya ujenzi wa vituo vya afya kwenye tarafa zisizo na vituo vya afya vyenye uwezo wa kutoa huduma ya upasuaji.**

Katibu aliwasilisha taarifa ya ujenzi wa vituo viwili vya Afya, wajumbe baada ya kupitia taarifa hiyo walijadiliana kwamba. Hadi sasa Halmashauri imepokea jumla ya Tshs. 500,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya. Ambapo fedha hizi zimegawanyika katika Majimbo (Jimbo la Morogoro Kusini Tshs. 250,000,000.00, Jimbo la Morogoro Kusuni - Mashariki Tshs. 250,000,000.00

Katika kuwasiliana na kupata maoni ya Waheshimiwa Wabunge husika mapendekezo ya maeneo ya Ujenzi ya Vituo hivi ni kama ifuatavyo:

- i. Kituo cha Afya katika Jimbo la Morogoro Kusini kijengwe kata ya Kasanga
- ii. Kituo cha Afya katika Jimbo la Morogoro Kusuni - Mashariki kijengwe kata ya Mkulazi

Halmashauri ilipokea barua yenye kumb Na.161/164/01/68 ya tarehe 25.10.2021 inayotoa maelekezo ya ujenzi wa Vituo vya Afya kwenye Tarafa zisizo na vituo vya Afya katika Halmashauri zetu.

### **Hitimisho**

Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango baada ya kupitia maelekezo ya ujenzi wa vituo vya afya kwenye tarafa zisizo na vituo vya afya vyenye uwezo wa kutoa huduma ya upasuaji na kutoa maamuzi kwamba kwa jimbo la Morogoro Kusini kituo kijengwe Korelo kwa sababu kitakuwa na uwezo wa kuhudumia wakazi kutoka Kasanga, Bungu na Kolero yenyewe. Kituo cha Afya kwa upande wa Morogoro Kusini Mashariki kijengwe Kata ya Mkulazi kwa sababu ya umbali wa kutoka Mkulazi hadi Ngerengere na kitakuwa na uwezo wa kuhudumia wakazi wa Kata ya Matuli, Mkulazi na ni eneo la kimkakati kwa ajili ya uwekezaji wa shamba la miwa.

### **Muht. Na. 03/12/11/2021 - Taarifa ya maandalizi ya Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022.**

Katibu aliwasilisha taarifa ya maandalizi ya Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022. Aliwaeleza wajumbe kwamba Halmashauri imeanza maandalizi ya Sensa ya watu na makazi ya Mwaka 2022 inayotarajiwa kufanyika mwezi Agosti 2022 kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Hadi sasa maandalizi yameshaanza ikiwa ni pamoja na kufanya kazi zifuatazo.:

- i. Kutambua takwimu za kaya
- ii. Kuunda kamati za uhamasishaji Sensa ya watu na makazi ya 2022



*Mh. C.P. Mboma* alieleza kwamba kuna mambo ya msingi yalitakiwa kutafutiwa ufumbuzi katika jengo la utawala. Mhandisi wa ujenzi alieleza kwamba majibu yaliwasilishwa kutoka kwa Mhandisi wa mkoa kuendelea na ujenzi kwa kuongeza ukubwa wa vyumba na unene wa ukuta wa ndani uwe sm 15 badala ya 25. Baada ya maelezo hayo walikubaliana kwamba Mkurugenzi Mtendaji ahamie katika jengo la utawala ili kuhimiza ujenzi uendelee kwa kasi.

*Mh. A. A. Mwamilang'anga* alitaka kujua kuna mpango gani wa upatikanaji wa vifaa kwa ajili ya Ujenzi huo. Mkurugenzi Mtendaji aliwaeleza wajumbe kwamba tayari mchakato wa nondo na mbao unaendelea na kokoto ziko eneo la ujenzi. *Mh. C.P Mboma* aliomba kuwe na mafundi wengi ili kumaliza kazi kwa wakati.

### **Azimio**

Shule ya Sekondari Kinole ujenzi wa madarasa Mkaguzi wa ndani aende kukagua thamani ya fedha ya ujenzi wa madarasa hayo.

Mwenyekiti alieleza kwamba kulikuwa na deni la Salmi ni Tshs 9,000,000.00 ni la muda mrefu la ujenzi wa madarasa shule ya Sekondari Matuli naye alipwe fedha zake. Ni mvumilivu sana. Kwenye mpango wa kulipa madeni na deni la Salmi liwepo.

*Mh. A. A. Mwamilang'anga* alizungumzia deni la walinzi wa masoko ya Tawa na Kinole hawajalipwa na kufanyike utaratibu wa kuondoa maji machafu yanayotiririka kwani hayana sehemu maalum pa kuyakusanya.

### **Muht. Na. 03/18/11/2021 - Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti**

Hapakuwepo na mengineyo yaliyojitokeza

### **Muht. Na. 03/19/11/2021 - Kufunga kikao**


Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufunga kikao, Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa ushirikiano waliouonyesha. Kabla ya kufunga kikao Mwenyekiti alizungumzia mambo yafuatayo; -

1. Viwanja vya Mvuha barabara zisafishwe ili viweze kuuzwa.
2. Maandalizi ya ujenzi wa stendi ya Mikese yafanyike ili ujenzi uweze kuanza.
3. Eneo la ekari 5 kwa ajili ya kugesha magari makubwa katika eneo la Gwata lifanyiwe kazi.
4. Suala la ukaguzi wa ndani kwa wodi 3 za wagonjwa lifanyiwe kazi na kuweza kujua nani kasababisha fedha kuliwa na mfumo. Nini kilipungua hadi kufikia hatua ya kutokamilisha majengo ya wodi tatu, kama imesababishwa na mtu hatutasita kuchukua hatua.
5. Iwasilishwe mikataba ya mafundi iliyosainiwa baada ya maamuzi ya baraza la Madiwani. Maagizo lazima yatekelezwe.
6. Kila mmoja atekeleze majukumu yake na kwa nafasi yake.




7. Kitengo cha ukaguzi wa ndani kinafanya kazi nzuri sana. Kama hatuna Imani na Mkaguzi wa ndani tuombe mkaguzi wan je kwa ajili ya wodi 3 za wagonjwa Hospitali ya Wilaya.
  8. Halmashauri iongeze nguvu katika ukusanyaji wa mapato.
  9. Idara ya Maendeleo ya Jamii wamazunguuka sana katika kukagua vikundi na mgawanyo wa fedha utawasilishwa katika kikao kijacho.
  10. Afisa Utumishi apange ziara ya kutembelea watumishi katika vituo vyao
  11. Afisa usafirishaji asimamie magari na taarifa iwasilishwe katika kikao kijacho
- Baada ya kusema hayo Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe na alifunga kikao mnamo wa saa 10:24 jioni.

**UMETHIBITISHWA.**



**KATIBU**  
*Rehema S. Bwasi*



**MWENYEKITI**  
*Lucas J. Lemomo*

06-12-2021

**TAREHE**